ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

## TAARIFA KWA UMMA

# MAKUSANYO YA KODI KWA MWEZI WA MACHI 2026

**Zanzibar, 02 April, 2026:**

## 1. MAKUSANYO YA MACHI 2026

Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), unawataarifu Walipakodi na Wananchi wote wa Zanzibar kwamba katika Mwezi wa Machi 2026, ZRA ilikadiriwa kukusanya **Tshs. 92.292 Bilioni**, na **IMEFANIKIWA** kukusanya Jumla ya **Tshs. 100.606 Bilioni**, ambao ni **UFANISI** wa **asilimia 109.01** wa Makusanyo ya mapato yaliyotarajiwa kwa Mwezi huo.

Aidha, Makusanyo hayo yakilinganishwa na Makusanyo halisi ya mwezi Machi ya Mwaka wa Fedha uliopita wa 2024/2025, ambayo yalikuwa ni **Tshs 73.750 Bilioni**, kuna **ONGEZEKO** la Makusanyo ya **Tsh 26.856 Bilioni** sawa na **UKUAJI** wa Makusanyo halisi wa **asilimia 36.42** (Jedwali Na. 1 linatoa ufafanuzi zaidi)

*Jedwali Na. 1: Makusanyo ya Mapato katika Mwezi wa Machi kwa Mwaka 2024/2025 na 2025/2026.*

| | 2024/2025 | 2025/2026 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwezi** | **Makusanyo (Tshs. Bilioni)** | **Makisio (Tshs. Bilioni)** | **Makusanyo (Tshs. Bilioni)** | **Ufanisi (%)** | **Ongezeko (Tshs. Bilioni)** | **Ukuaji (%)** |
| Machi | 73.750 | 92.292 | 100.606 | 109.01 | 26.856 | 36.42 |

*Chanzo: Mamlaka ya Mapato Zanzibar, 2026.*

## 2. MAKUSANYO YA ROBO YA TATU (JANUARI - MACHI 2026)

Katika kipindi cha Robo ya Tatu ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, ZRA ilikadiriwa kukusanya **Tshs. 344.633 Bilioni**, na **IMEFANIKIWA** kukusanya Jumla ya **Tshs.320.480 Bilioni**, sawa na wastani wa makusanyo ya **Tshs. 106 Bilioni** kwa Mwezi.

Kwa kulinganisha na Makusanyo ya Robo ya Tatu ya Mwaka uliopita wa 2024/2025, ambayo yalikuwa ni **Tshs. 238.746 Bilioni**, yanaonesha **ONGEZEKO** la Makusanyo ya **Tshs 81.734 Bilioni** sawa na **UKUAJI** wa Makusanyo ya **asilimia 34.23**.

## 3. SABABU ZA KUFANYA VIZURI:

Ufikiaji wa lengo la Makusanyo ya Kodi kwa **asilimia 109.01** ni pamoja na mambo mengine umesababishwa na:

i. Uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu na huduma za kijamii pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi Zanzibar unaotokana na utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

ii. Kuimarika na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, zinazotokana na sera na uongozi mzuri wa **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zilizoimarisha mazingira ya biashara kwa pande zote mbili za Muungano.
iii. Kuongezeka kwa Muitikio na uhiyari wa kulipa kufuatia mazoezi ya elimu kwa walipakodi ikiwemo Kampeni ya **ZRA mtaani kwako**.
iv. Kuwepo kwa Matokeo chanya yanayotokana na Zoezi la **KUUNGANISHA MIFUMO** kati ya Mifumo ya Walipakodi na Mifumo ya ZRA hasa katika biashara ya Hoteli za Kitalii.
v. Kuongezeka kwa Usajili wa walipakodi wapya wakiwemo wafanyabiashara wa kimataifa wanaofanya biashara Zanzibar.
vi. Kuimarika kwa uingiaji wa watalii Nchini kunakochochewa na uwepo wa utulivu na mazingira wezeshi ya kibiashara na kiutalii.
vii. Kuimarika kwa ushirikiano baina ya Wizara na Taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) sambamba na kuimarika kwa Mahusiano na Ushirikiano kati ya ZRA, Wafanyabiashara na wadau wengine kulikopelekea kuongezeka kwa ulipaji kodi wa hiari .
viii. Kuimarika kwa **UWAJIBIKAJI NA WELEDI** kwa Watumishi wa ZRA kunakopelekea uthabiti katika usimamizi na ukusanyaji wa mapato.

## 4. MIKAKATI YA UKUSANYAJI KWA ROBO YA NNE (APRILI - JUNI 2026) :

Katika kuendelea na jukumu la ukusanyaji wa Mapato ya Serikali, na kukamilisha ukusanyaji wa Mapato ya Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, kwa Kipindi cha Robo ya nne (Aprili – Juni 2026) ZRA itaendelea kutekeleza mikakati ifuatayo:

I. Kuongeza kasi katika kuhakikisha Mifumo yote ya Kibiashara ya Walipakodi inaunganishwa na Mifumo ya ZRA.
II. Kuendeleza utaratibu wa utoaji wa huduma za Kodi kwa ukaribu kwa Walipakodi wa makundi tofauti sambamba na kuweka Kambi katika maeneo ya karibu na biashara ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za Kodi kwa Walipakodi.
III. Kusimamia kwa ufanisi na kukamilisha kazi ya ukaguzi wa Walipakodi ambao wamepagwa kufanyiwa ukaguzi ndani ya Mwaka wa Fedha 2025/2026.
IV. Kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa Miradi yote ya Serikali ambayo ujenzi wake unaendelea ili kuweza kufahamu na kukusanya kiwango sahihi cha Kodi ambayo Serikali inalipa kupitia Miradi hiyo.
V. Kuongeza kasi ya kufanya mazoezi mbali mbali ya kuhamasisha uwajibikaji wa hiyari kwa Walipakodi na kuwachukulia hatua Walipakodi ambao watashindwa kutekeleza wajibu wao wa kisheria.

## 5. HITIMISHO:

Mamlaka ya Mapato Zanzibar inawashukuru Walipakodi wote kwa kushikamana na ZRA sambamba na kutekeleza wajibu wao wa kisheria wa kuwajibika katika ulipaji Kodi kwa hiyari.

Ili kufanikiwa katika kulifikia lengo la makusanyo ya Robo ya Nne (Aprili – Juni 2026) na kukamilisha makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa mafaniko, ZRA inawahimiza Walipakodi wote ambao wanatumia mifumo katika uendeshaji na usimamizi wa biashara zao, kuhakikisha wanakamilisha uunganishaji wa Mifumo hiyo na Mifumo ya ZRA Ndani ya Mwezi wa Aprili 2026.

**"Tulipe Kodi Kwa Maendeleo ya Zanzibar"**

**Makame Khamis Moh'd**
**Mkuu wa Kitengo cha Habari, Uhusiano na Huduma kwa Wateja**
**Mamlaka ya Mapato Zanzibar**